# Ni maji yetu pia!

## Kuleta usawa katika upatikanaji wa maji nchini Kenya





## 1. Utangulizi

Nchini Kenya, kila mwananchi ana haki ya kupata maji. Mkakati wa taifa wa maji umedhamiria kuhakikisha kwamba watu wote wanafikiwa na mfumo rasmi wa usambazaji wa maji, na masikini wa Kenya wanalipa gharama za maji ambazo wanaweza kumudu.

Hatua ya kuridhisha imepigwa na kuwezesha upatikanaji wa maji tangu kupitishwa kwa sheria ya maji ya mwaka 2002. Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji yaliongezeka kutoka KSh bilioni 6.9 mwaka wa fedha 2004/5 hadi Ksh bilioni 18.6 mwaka 2008/9. Kwa kuangalia ongezeko la matumizi, kiasi cha uwekezaji kilichopo (bajeti ya maendeleo) kiliongezeka karibu mara tatu kutoka Ksh 140 kwa kila Mkenya hadi Ksh 391 (GOK, AWSR 2009). Wakati huo huo, mabadiliko ya sera yaliyotenganisha umiliki wa miundombinu kutoka utoaji huduma, kanuni na utungaji sera yalifanyika.

Licha ya maendeleo haya ya mazuri, bado mengi yanahitaji kufanywa. Mamilioni ya wakenya kwa sasa hawapati huduma ya  maji, na wananchi wengi wanaendelea kunywa maji yasiyo salama, au wanalazimika kutumia kiasi kidogo sana cha maji kutokana na umbali, muda wa kusubiri ili kuteka maji na gharama za kuyapata maji. Tofauti kubwa sana ipo katika hali ya upatikanaji wa maji, na jitihada za kutafuta maji kwa baadhi ya wakenya wasiofikiwa na huduma hiyo, zinatofautiana mno zikilinganishwa na waliopendelewa kupata huduma ya maji, ambao maji huwafikia nyumbani kwao, na mara nyingi kwa gharama ndogo tu.

Kijarida hiki kinawasilisha mambo- manane kuhusu maji nchini Kenya. Kwa kasi ya sasa ya upanuzi wa huduma za maji kwa umma, itachukua kipindi kirefu sana kuzifikia jamii zote zilizo na mahitaji makubwa ya maji. Serikali inahitaji kushughulikia kwa haraka tofauti zilizopo katika hali ya upatikanaji wa maji, hasa kwa kuhakikisha kuwa mgawo wa bajeti unafanyika kwa kanuni zinazozingatia mahitaji na usawa zaidi kuliko uzito wa kisiasa na upendeleo kwa matabaka ya juu.

Uwazi
pata picha kamili

Kijarida hiki kiliandaliwa na Uwazi-Twaweza
iliyopo Hivos.

Uwazi, SLP 19875 – 00202 Nairobi, Kenya.
Simu +254 20 386 1372/3/4
Baruapepe: info@uwazi.org. tovuti : www.uwazi.org
Imetolewa Novemba 2010


# 2. Mambo 8 kuhusu upatikanaji wa maji nchini Kenya

## 1: Mamilioni ya wakenya wanapata maji yasiyotosheleza mahitaji

Taarifa za kuaminika juu ya hali halisi ya upatikanaji wa maji salama kwa umma hazipatikani kwa urahisi. Hata makadirio yaliyopo ya asilimia ya kaya za mijini zilizo na vyanzo vya maji safi na salama zinataofautiana sana. Katika kijarida hiki tunatumia takwimu zilizokusanywa na Benki ya Dunia ambayo inawasilisha seti mbili za makadirio (World Bank 2009). Makadirio haya yanayaweka maji yote yanayosukumwa kwa bomba kuwa ni kati ya asilimia 42 na 59, ambapo inawaacha mamilioni ya wananchi bila kuwa na maji yanayopatikana kiurahisi. Hata kwenye makadirio ya juu zaidi, karibu wakenya milioni 16 wanategemea maji ya vibandani, visimani, maji ya mvua, na vyanzo vya maji vya wazi kama vile mito na visima vifupi ili kukidhi mahitaji yao ya kila siku.

Mbali na makadiro hayo, maeneo ya vijijini siku zote yana hali mbaya zaidi yakilinganishwa na mijini. Katika maeneo ya vijijini ambako wakenya asilimia 78 wanaishi, ni asilimia 38 hadi asilimia 52 tu wanaopata maji salama kiurahisi; maeneo ya mijini asilimia 59 hadi 83 wanapata maji salama (Benki ya Dunia 2009). Hata ndani ya maeneo ya mijini, kuna tofauti kubwa za upatikanaji maji kati ya kaya masikini na zile zenye uwezo mkubwa kiuchumi. Kwa mujibu wa ripoti ya zoezi la Pimakadi ya umma la mwaka 2007 (CRC, 2007), ni kaya chache sana (2%) zisizo masikini jijini Nairobi zinazotegemea maji ya vibandani, lakini zaidi ya robo tatu (36%) ya kaya masikini zinategemea chanzo hicho. (mchoro 1).

**Mchoro 1: asilimia ya kaya masikini na zisizo masikini zinazotegemea vibanda kama chanzo cha maji yao**





**Chanzo cha takwimu:** Pimakadi ya Umma kuhusu Maji mijini (CRC), 2007

## 2: Vibanda vya maji mjini vinatoa huduma ya maji isiyotosheleza

Kwenye maeneo ya mijini, asilimia kubwa ya kaya zinapata maji ya bomba, lakini bado wengi wanalazimika kutegemea maji ya vibandani, mathalan (kaya 15% Nairobi; kaya za Kisumu na Mombasa 45%). (CRC 2009). Hali hii inaleta mzigo mkubwa kwenye kaya maana uchotaji maji unatumia muda wingi. Kwa kawaida kaya huchota maji safari 4-6 kwa siku; hivyo, hata kama kibanda cha maji kikiwa karibu na kaya bado wananchi hutumia muda mwingi kupata maji. Mjini Nairobi, kaya zinazotegemea vibanda vya maji hutumia dakika 54 kwenda kibandani kwa msimu

wa kawaida, na zaidi ya mara mbili ya muda huo (dakika 126) wakati wa uhaba wa maji. Katika maeneo mengine hali ni mbaya zaidi. Kwa mfano, Kisumu kaya zinazotegemea maji ya vibandani zinatumia karibu ya saa mbili (dakika 112) kuchota maji kila siku za kawaida, na katika misimu ya uhaba hutumia  zaidi ya saa tatu (dakika 200). Zaidi ya hayo, kwa sababu wanawake ndio wabeba jukumu kubwa la kuchota maji, uhaba wa maji unaongeza uwepo wa tofauti kubwa za kijinsia.

**Mchoro 2: Muda unaotumiwa kila siku na kaya masikini kuchota maji toka vyanzo vya maji mbali na nyumba zao**





**Chanzo cha takwimu:** Pimakadi ya Umma (CRC), 2007

## 3: Watu masikini maeneo ya mijini wanagharimika zaidi ilikutumia maji

Uwekezaji usiozingatia haki na ukarabati duni wa mabomba ya usambazaji maji vimesababisha wananchi kushindwa kumudu gharama za maji. Kwenye makazi ya mabanda mijini, masikini wananunua maji kwa gharama kubwa mara kadha kuliko gharama wanazolipa watumiaji wasio masikini na wenye maji ya bomba nyumbani. Zaidi ya hili, usambazaji wa maji kwenye mitaa ya mabanda sio wa kutegemewa, na kukosekana kwa maji ni kitu cha kawaida. Matokeo yake ni kwamba wale wenye uwezo mdogo zaidi wa kulipia huduma za majiwanalipa bei kubwa mno na bado wanaendelea kupata maji kwa taabu.

**Mchoro 3: Wastani wa kiasi kinacholipwa kwa lita 1,000 kutoka mtandao wa mabomba na maji ya vibanda**




**Chanzo cha takwimu:** PimaKadi ya Umma, juu ya maji mjini (CRC), 2007

Kwa mujibu wa utafiti wa Pimakadi (*citizen report cards*) watu wa maeneo ya mijini wanaopata maji kutoka vibanda vya maji, wanalipa hadi zaidi ya mara tano ya wale wanaopata maji yao nyumbani kutoka kwenye mtandao wa mabomba. Lakini huenda hali ni mbaya zaidi kuliko taarifa inavyoonyesha. Kwa mfano mtaa wa mabanda wa Kibera, Nairobi, wakazi mara nyingine wanalipa hadi mara 30 zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikilinganishwa na kiasi kidogo wanacholipa watu wa tabaka la kati na wale wenye kipato cha juu (angalia kisanduku 1).

**Kisanduku 1: Wakenya masikini wanalipa zaidi kwenye maji**

Bw Ngarama, mkazi wa mtaa wa mabanda wa Kibera, Nairobi, anaeleza: "natumia karibu makontena 40 ya ndoo za ujazo wa lita 20 (lita 800 za maji) kwa mwezi kwa familia yangu ya watu watano. Tunatumia maji hayo kwa ajili ya usafi, kupikia na kunywa. Inanigharimu kati ya Sh za Kenya 200 hadi 400 kwa mwezi, kutegemeana na msimu. Maji hayatoshelezi mahitaji yetu, lakini kama tunahitaji zaidi, napaswa kutumia fedha zaidi. Lakini sina fedha za kukidhi mahitaji yote ya maji ya familia yangu, kwa maana wote tunategemea kipato kidogo cha Sh 2,000 za Kenya kugharamia chakula, kodi ya nyumba na mahitaji mengine ya familia."

Yakobo, ni mkazi wa Kilimani, eneo la watu wenye hali ya kati, kama kilomita 2 kutoka Kibera, anaishi na familia yake ya watu watatu. Wanatumia wastani lita 9,000 za maji kwa mwezi. Wanatumia maji kufulia nguo, kusafisha nyumba, kupikia, kuogea, kumwagilia miti na kuoshea magari. Eneo hilo la jirani limewekewa mita za kuhesabu ujazo wa maji yanayotumika, na Kampuni ya Maji Nairobi humdai kiasi cha fedha ya Kenya Sh 12 kwa kila lita 1000 za maji, hivyo, kwa wastani Yakobo hulipa Sh 108 kila mwezi.


Ukilinganisha wakazi hawa wawili wa Nairobi, huyu masikini, asiye na mita Bwana Ngarama analipa wastani wa Ksh 0.375 kwa lita moja ya maji, karibu mara 30 ya kiasi anacholipa tajiri mwenye mita bwana Yakobo anayelipa kiasi cha Ksh 0.012 tu kwa lita.

**Chanzo:** Mazungumzo binafsi ya mfanyakazi wa Uwazi, Nairobi, Septemba 2009.

## 4: Itachukua miaka 30 kwa vijiji kupata usambazaji maji kwa watu wengi

Upatikanaji wa vyanzo vya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ni mdogo. Upatikanaji umeongezeka taratibu kwa kipindi fulani kwa kiwango cha karibu pointi ya asilimia 1 kwa mwaka.

**Mchoro 4: Mwelekeo wa utumiaji maji salama kwenye maeneo ya vijijini**





**Chanzo cha takwimu:** Benki ya Dunia, 2010

Kwenye mikataba ya huduma inayotumiwa maeneo ya mijini, *usambazji wa maji kwa umma unaokubalika* unaangaliwa kwa uwepo wa angalau 80% ya watu wanaopata maji ya kunywa yaliyo salama na ya kutosha. *Usambazaji muafaka na bora zaidi* unaangaliwa kwa kuwa na angalau 90% ya watu wote katika nchi kupata maji safi, salama na kwa njia rahisi. Kama vigezo hivi vikitumika na kutumiwa kama matarajio mazuri ya upatikanaji maji maeneo ya vijijini nchini Kenya (ukweli wa 1), itachukua miaka mingine 30 au zaidi hadi kufikia viwango vinavyokubalika vya uenezaji na usambazaji wa maji kwa jamii pana maeneo ya vijijini, na miaka mingine 40 au zaidi kufikia viwango vya usambazaji muafaka.

## 5: Hata mijini upatikanaji wa maji kwa umma unapungua

Kwenye maeneo ya mijini, mwelekeo unatisha maana upatikanaji wa maji salama umekuwa ukipungua kadiri siku zinavyokwenda. Ingawa upatikanaji wa maji safi na salama uko kwenye 84% (makadirio mazuri), ni wazi kwamba mwelekeo wa upatikani maji unahitaji kuboreshwa zaidi. Hadi sasa, uwekezaji kwenye ugawaji maji mijini bado haufuati kanuni inayoambatana na ongezeko kubwa la idadi ya watu mijini. Zaidi ya hili, asilimia kubwa ya miundo mbinu maeneo ya mijini haifanyi kazi (Nairobi 56%; Kisumu 26%; Mombasa 38%). Hii ina maana kuwa usambazaji wa maji mijini unaweza kuwa chini zaidi ya viwango rasmi vinavyoripotiwa na taasisi husika za huduma za maji. Hali ya usambazaji inadhoofika zaidi kwa wakazi wa mijini, maana kuna maji mengi zaidi yanayopotea hovyo-kupitia kuvuja kwenye nyufa au matundu, uunganishaji maji haramu na usambazaji ulioingiliwa na rushwa. Nairobi inaonyesha kuna upotevu hovyo wa maji asilimia 40%; Kisumu 66%; Mombasa 35%) (CRC 2007). Viwango hivi ni vya juu zaidi, havikubaliki na ni kinyume na malengo ya sera ya kitaifa ya maji.

**Mchoro 5: Mwelekeo wa utumiaji maji salama kwenye maeneo ya mijini**




**Chanzo cha takwimu:** Benki ya Dunia, 2010

## 6: Huduma zinazotolewa na wasambazaji maji hazitoshelezi

Licha ya matamko na sera nzuri zinazoahidi wananchi kupatiwa huduma bora ya maji toka taasisi za kuhudumia maji, kiwango cha huduma kwa wananchi bado kinasuasua. Kaya nyingi, zote za masikini na wasiokuwa masikini, zinapata tatizo la uhaba wa maji hata kama ziko ndani ya


maeneo ambayo yana mitandao ya maji au kwenye viunganishi vikuu na vibanda vya maji.

Kwa mfano, hata pale maji yanapotolewa kupitia mabomba, asilimia 13 – 42 ya watu wasio masikini na asilimia 19 – 44 ya kaya masikini maeneo ya mijini wanaripoti uhaba au kukosekana kwa maji. Uhaba wa maji mara nyingi unatokana na kukatwa maji mara kwa mara kwa zaidi ya saa 24 kwa kaya zilizounganishwa na mabomba (Mchoro 6).

Ili kukabiliana na uhaba wa maji, familia nyingi zinaingia gharama zaidi ya kununua na kujenga mabirika ya kuhifadhia maji. Wale ambao hawawezi kumudu gharama za kufanya hivyo wanalazimika kuishi bila maji ya kutosha, kutumia maji yasiyo salama, au kulipa fedha nyingi zaidi kwa ajili ya maji kidogo yanayopatikana.

Kukosekana kwa ukarabati au ukarabati duni wa mitandao ya usambasazi , pamoja na rushwa katika huduma za maji ni visababishi vikuu vya uhaba wa maji. Ukiritimba wa makampuni machache ya maji, unaoonekana kuchangiwa na ushirikiano wa kifisadi kati ya maafisa wa serikali na waKampuni za Majivinaendeleza uhaba bandia wa maji kwa manufaa yao binafsi. Wakati baadhi ya wauza maji ni wajasiriamali halali, wengine ni maafisa wa taasisi za huduma za maji ambao huchukua maji kutoka mikondo ya umma ya usambazaji na kuyauza kwa wananchi wasiopata maji au wanaopata maji kidogo kwa bei ya juu kuliko bei ya maji wanayolipa kaya zilizounganishwa. Kiasi cha maji kinachoonyeshwa kuwa matumizi yake “hayajulikani” (47% kwa mujibu wa Benki ya Dunia, 2009) inawezekana mara nyingine, sehemu kubwa huchukuliwa kupitia njia hizi.

**Mchoro 6: Asilimia ya kaya za mijini zinazotumia maji ya bomba kwa kunywa, zinazoathiriwa na uhaba wa maji**




**Chanzo cha takwimu:** Pimakadi ya Jamii, kuhusu maji mjini, 2007

**Kisanduku 2: Wadaiwa masikini na utaratibu wa ukusanyaji ankara**

Nilihamia nyumba hii miaka minne iliyopita. Wakati nasaini nyaraka zangu za upangaji, pia nililipa kwa Wakala wa Usimamizi wa Mali ada ya maombi ya akaunti ya malipo kwa Kampuni ya Maji ya Nairobi

Wiki mbala baada ya kuhamia, maafisa kutoka Kampuni ya Maji Nairobi walifika kwa ukaguzi wa kawaida na wakakata maji kwenye nyumba yangu. Pia waliacha ujumbe ulioandikwa kwenye kipande cha karatasi kuwa nadaiwa na Kampuni ya usambazji maji (NWS) jumla ya Ksh 98,000. Na walisema wazi kuwa hawatarudisha huduma ya maji hadi hapo deni litakapolipwa.

Niliwaambia kuwa nimeishi hapa kwa wiki mbili tu na kwa namna yeyote deni hilo la maji haliwezi kuwa langu! Waliondoka bila kunisikiliza kikamilifu. Mmoja kati yao alinivuta pembeni na kunieleza kuwa wangeweza kuunganisha na kurudisha huduma kama ningewapatia '*chakula kidogo*'. Niliamua kutotoa hongo lakini nikafuatilia suala hili kiofisi kupitia wakala wa mali.

Saa moja tu baada ya kuongea na wakala, huduma ilirudishwa. Wakala wa Mali walinihakikishia kuwa suala hili limekwishatatuliwa na taarifa za akaunti yangu mpya zingetumwa mara, kabla ya mwezi kuisha. Mwezi ulipita na hakuna kilichokuja. Huduma ya maji ikakatwa tena, katika mazingira yaleyale. Niliwapigia simu wakala na huduma ikarudishwa. Ankara yangu ya maji kamwe haikuletwa.

Niliamua kufuatilia jambo hili kwenye ofisi ya NWC. Hapo ndipo nikagundua tatizo la ankara za maji la nyumba hii ni la zaidi ya miaka 11. Kampuni ilikuwa na mgogoro na mwenye nyumba kuhusu ankara za maji tangu nyumba ilipojengwa. Mimi nilikuwa mpangaji wa nne na hakuna hata mpangaji mmoja wa nyuma aliyekuwa na akaunti. Hivyo, hakuna hata mmoja kati yao aliyelipia maji aliyotumia!

Kampuni ilikataa kunianzishia akaunti mpya ili nianze kulipia matumizi yangu ya maji hadi deni la zamani litakapolipwa. Nimekwisha jaribu kuwaeleza utayari wangu kuanza kulipa wakati wanatatua deni lililopo, lakini maafisa wa kampuni wameendelea kukataa. Kwa kipindi chote hiki, wameendelea kuja mara kwa mara kukata maji. Na mimi kama kawaida nawapigia Wakala wa Mali na tatizo linatatuliwa kwa muda

Mara ya mwisho nilikagua deni la malipo ya maji kwa nyumba hii, limeshafikia Ksh. 224,000. Naihurumia Kampuni kwa hasara zote inazopata kwa sababu ya deni la nyuma lisilotarajiwa kulipwa. Nimechoka na usumbufu wa kukatiwa maji. Ninahamia nyumba nyingine ambayo haina tatizo".


*Mulandi, Mkazi wa Nairobi*

**Chanzo:** Mazungumzo binafsi na mfanyakazi wa Uwazi, Nairobi, Septemba 2009.

## 7: Mgawo wa bajeti hauendani na mahitaji

Fedha za uwekezaji katika sekta ya maji zinagawanywa kwa namna ambayo haiwiani na mahitaji. Mathalani, kwa mujibu wa Benki ya Dunia, uwekezaji uliopangwa kwa ajili ya maji maeneo ya vijijini ulikuwa pungufu kwa asilimia 54-57 ya mahitaji halisi ili kufikia kiwango cha huduma ya maji cha Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Kwa upande mwingine, kwenye maeneo ya mijini uwekezaji uliopangwa ulizidi kiasi kinachohitajika kwa asilimia 10-19!

**Mchoro 7: Uwiano baina ya Uwekezaji unaohitajika na uliopangwa kwenye maji mijini na vijijini**




**Chanzo cha takwimu:** Benki ya Dunia, 2010

Bajeti pekee inayozingatia mahitaji ni fedha inayotengwa na Wakfu wa Huduma za Maji (WSTF). Wakfu huu wa kitaifa ulianzishwa maalumu ili kuongeza uenezaji maji kwenye maeneo yasiyohudumiwa vya kutosha, chini ya Mpango wa Uwekezaji Maeneo Masikini sana (PPIP). WSTF huzigawa fedha zake kwa kuangalia mambo matatu: hali ya umaskini kijiografia, mashauriano/maelekezo ya wananchi, na vipaumbele vya kisiasa (AWSR 2009). Kwa bahati mbaya, mbinu hii imeacha mawanda mapana ya uingiliwaji na ushawishi wa mababe wa kisiasa. Zaidi ya hili, WSTF inapata bajeti ndogo chini ya 1% ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya Taasisi za huduma ya Maji (AWSR 2009), na hivyo hakuna uhakika kwamba mapambo ya matamshi ya nia njema kuhusu kuwahudumia vyema zaidi jamii maskini yanaambatana na vitendo.

## 8: Inawezekana Kupanga bajeti ya sekta ya maji kwa kuzingatia vigezo

Kwa kuangalia hali ya sasa ya kutokuwepo usawa kwenye upatikanaji wa maji, mgawo wa bajeti na hitaji la kuongeza kasi ya uwekezaji ili kufikia kiwango kinachokubalika cha usambazji maji, hatua moja mbele ingepigwa iwapo bajeti iliyoongezwa kwa ajili ya huduma za maji ingegawanywa kwa namna isiyo na upendeleo na namna inayokuza haki. Hili linaweza kufanyika kwa wizara husika kuamua kutumia mfumo wa ugawaji fedha unaotumia kanuni.

Kwa muda mrefu,mgawo wa bajeti unaozingatia vigezo maalumu kwenye sekta ya maji ulikuwa unazuiliwa na kukosekana kwa takwimu, kama ilivyooneshwa na mkanganyiko kuhusu viwango halisi vya uenezaji maji kama kwenye mchoro 1. Lakini, kwa sababu Sensa ya idadi ya watu ya mwaka 2009 iliuliza maswali kuhusu vyanzo vikuu vya maji vya kaya ikiwa na vipengele 15 tofauti vya kujibiwa, suala hili limetatuliwa kwa kiwango kikubwa. Sasa inawezekana kujua na kuwa na uhakika kuhusu idadi ya watumiaji wanaotegemea vyanzo visivyo salama vya maji, kupitia mikoa na hata katika ngazi za chini zaidi za kijiografia. Na hizi ndizo zinapaswa kuwa misingi muhimu ya kanuni ya kupanga bajeti ya maji.

Vigezo vingine vinavyopaswa kuzingatiwa ni pamoja na utajiri (au umasikini) kijiografia na utendaji wa watoa huduma za maji. Utendaji wa taasisi za huduma utasaidia kuepuka hali ya zamani ambapo kwa mfano Shirika la Taifa la Hifadhi ya Maji na Mabomba (NWCPC) lililokuwa limetawaliwa na rushwa lilipokea kutoka serikalini kiasi cha 99% cha bajeti yake ya Ksh milioni 4,369.2 wakati maafisa wake waliokuwa wanatuhumiwa kwa ufisadi mkubwa wakiwa bado madarakani na hawajachukuliwa hatua za kisheria.

Taarifa kuhusu utajiri/umaskini na utendaji wa taasisi za huduma za maji kwa sasa zinapatikana pia. Ramani ya kitaifa ya hali ya umaskini inatoa viashiria vizuri kuhusu mahali walipo watu wengi masikini. Vile vile baadhi ya taarifa kuhusu ufanisi wa watoa huduma za maji zinaweza kupatikana kutoka kwenye Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka ya Sekta ya Maji.

# 3. Hitimisho

Ripoti hii imeonyesha kwamba karibu miaka 50 baada ya uhuru, huduma ya maji imebaki kuwa changamoto kubwa nchini Kenya. Mamilioni ya Wakenya hawana maji tosha na salama, na kasi ya sasa ya maendeleo ya sekta hii haonyeshi matumaini ya kuwepo kwa upatikanaji wa kutosha wa maji salama kwa umma katika kipindi kifupi kijacho.

Bei za maji zisizo za haki zinawaumiza zaidi masikini; wale wanaomudu kiurahisi kulipa gharama za maji wanalipa fedha kidogo tu; wakati wale wanaomudu kulipia gharama kwa taabu sana wanagharimika zaidi katika nyanja za: fedha, muda mwingi, na afya zao wanapotumia maji kutoka vyanzo visivyo salama.

Serikali ya Kenya inafahamu hali hii, na kwa namna inayostahili pongezi, imeongeza bajeti kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji. Kwa bahati mbaya, vigezo ambavyo mgawo wa bajeti unazingatia vinategemea ushawishi wa kisiasa na taratibu ambazo hazileti usawa. Kwa hiyo, ongezeko la fedha haliwezeshi uboreshaji wa huduma za maji kwa wakenya wengi.

Hatua moja rahisi inapaswa kutekelezwa kama kipaumbele cha kupunguza tofauti zilizopo kwenye hali ya upatikanaji wa maji.

### *Anza kupanga bajeti kwa kuzingatia vigezo maalum*

Takwimu muhimu kwa ajili ya hivyo vigezo zinapatikana kutoka Sensa ya idadi ya watu ya 2009 na katika sura ya Taifa ya Umaskini. Taarifa za hali ya juu zaidi mathalani, ili kubaini ufanisi wa watoa huduma za maji na utendaji kazi wa Mitandao ya maji ya umma, zinaweza pia kutumiwa. Hakika, hatua thabiti zinawezekana – swali ni iwapo Wakenya na serikali yao watachukua hatua kuleta mabadiliko.

# Rejea


Water and Sanitation Program - Africa (2007). *Citizen Report Card for Water in Urban Areas.* Nairobi.

World Bank (2009). *Country Status Overview of Water Supply and Sanitation Kenya*, Consultation Draft, Nairobi.

World Bank (2010). *AMCOW Country Status Overview II: Kenya Briefing March*. Nairobi: World Bank.

Government of Kenya (GOK), Ministry of Water and Irrigation (2009). *Annual Water Sector Review (AWSR) 2009*. Nairobi: GOK.